Moto kutoka mbinguni

toka Jamhuri Kidemocratic ya Congo

Askari wa Kitutsi walivunja mlango nyumbani mwa mchungaji na familia yake. Askari hao waliwatisha wakiwaonyesha bunduki zao. Lengo lao lilikuwa wawamalize raia Kihutu kijijini. Yule mchungaji alilia akisema, “Jamani, hamtupi hata nafasi kidogo ya kusali mimi na familia yangu kabla hatujafa?” Askari hao walicheka kwa dhihaka sana walipotazama familia hiyo walivyopiga magoti kwa unyenyekevu na kuomba rehema za Mungu. Walakini hakuna risasi iliyofyatuliwa. Baada ya maombi yao, familia walisimama taratibu, wakakuta wale askari wameondoka, wamekwisha tokomea mbali na kile kijiji pia.

Baada ya miezi kadhaa walielewa kilichotokea. Katika mkutano wa kanisa kwenye mji mwingine, watu walikutana kwa ajili ya kuomba. Hapo huyo mchungaji alishuhudia jinsi Mungu alivyowahifadhi familia yake usiku huo, jinsi askari walivyotoweka kutoka katika nyumba yao na katika kijiji.

GHAFLA MOTO ULISHUKA

Ndipo akasimama mtu mmoja alitoka nyuma ya nyumba hio akisema, “Nadhani naweza kueleza ilivyotokea.” Huyo alikuwa mmoja wa askari waliokuwepo usiku huo nyumbani kwao ilipovamiwa. Akasema, “Ilikuwa hivi, nilikuwa pale tulipovunja mlango kuingia nyumbani mwako. Mimi ndiye niliyeamuru watoto wako wapange mstari na kutazama bunduki yangu mlipopiga magoti kuomba. Ghafla, ukuta wa moto mkali wenye cheche kali ulishuka na kuwafunika. Hatukuweza kuona ng’ambo ya moto ule. Kutokana na joto kali la ule moto tulijua kuwa nyumba yenu ingeungua mara moja, hivyo tukaondoka kwa haraka sana.

“Tulipotoka nje tuliona nyumba yako imefunikwa na moto lakini haikuteketea na kwa hiyo tuligundua ya kwamba haukuwa moto wa kawaida ule tuliouzoea bali ulikuwa moto uliotumwa na Mungu. Kama ni hivyo ndivyo Mungu wenu anavyojibu, basi hata mimi nataka kumjua. Nimechoka na mapigano na mauaji na ndio maana leo nimekuja kuungana nanyi.”

YESU alisema: Naja—

u p e s i

Ufunuo 22:12

Nilishikwa uwanjani mwa ndege

na Rafiki Mmoja — Sudan

Mimi nilizaliwa nchini Sudan yapata miaka thelathini iliyopita, nikiwa mwana wa nane kati ya watoto tisa. Babangu alikuwa wakili na baadaye akachaguliwa kuwa na vyeo mbali mbali katika serikali chini ya waziri. Kwa sababu ya vyeo hivyo alivyokuwa navyo aliuawa, pamoja na kaka zangu wawili na shemeji zangu, wakati wa vita vya mwaka wa 1992. Wakati huo sikuwa nchini mwangu.

Niliporudi Sudan mwaka wa 1994, nikiwa bado uwanjani mwa ndege nilishikwa na askari nao walinipeleka moja kwa moja kwenye kambi la jeshi ambapo niliteswa sana kwa kipindi cha miezi sita. Baadaye nikaachwa huru lakini nilikaa chini ya ulinzi mkali. Hali nchini Sudan ilikuwa imeharibika sana kwani njaa, magonjwa na mauaji yalizidi kila mahali. Wakristo wengi waliongoka kuwa waislamu kila siku kusudi wapokee chakula.

Miujiza kutoka kwa Yesu ilitendeka, nami niliweza kukimbilia Kenya katika mwaka wa 1995. Nikakaa kambini mwa wakimbizi katika Kenya kwa muda wa miaka mitatu na nusu. Nikajaribu kuwasaidia wakimbizi wengine nami mi hali kadhalika tupitie Care International. Nilipokuwa ningali hapo, miujiza mingi ilitendeka iliowasaidia wakristo wengi watambue kwamba Yesu Kristo pekee ndiye Mlinzi na Mwenye kuwahifadhi. Wakaelewa kwamba yote yanawezekana kwake Mungu Mwenyezi. Kwa sababu ya miujiza ambayo Yesu alikuwa akitenda katika Kambi ya Jamii ya Kisomali, watu wengi waliokoka na kumpokea Yesu kuwa Mwokozi wao.

Baadaye, Mungu alinisaidia niende Canada na sasa nafurahi. Kwa njia ya maombi, mamangu na dada zangu ambao bado wangali nchini Sudan, waliniandikia. Ninayo furaha kwamba Yesu ni Mwokozi wangu na rafiki ambaye hawezi kuniaibisha kamwe. Namsifu yeye kwani Bwana ni Mchungaji mwema.

Unaweza kuponywa

na Gewuma — Uganda

Nilijiuliza, “Ni kitu gani kinachonifanya nivimbe hivyo?” Watu walinishauri niende kumwona mganga wa kichawi ambaye angeweza kunisaidia. Nilipomwona huyo mganga aliniambia ya kwamba nimepooza na ingehitajika mbuzi mweusi auawe pamoja na kuku weupe watatu. Lakini hilo halikunisaidia lolote. Nilienda kumwona mganga mwingine naye alinituma nilete kuku weusi wawili na shilingi elfu moja. Hata hivyo bado sikupona.

Nilijiambia, “Ni lazima sasa niende kwenye hospitali ya Mbale.” Hata hivyo, baada ya kwenda bado hawakunisaidia wala hawakuweza kunitendea msaada lolote. Kwa hiyo niliamua kuwa ningekufa.

Nikiwa pale hospitalini Mbale mwuguzi mmoja alikuja pale nilipokuwa nimelala. Nilimwona akigawa karatasi kwa watu ambao aliwajua. Nilimwomba anipe moja naye akanipa. Karatasi hiyo ilikuwa imeitwa UPESI. Niliona ilifundisha jinsi Mungu alivyowasikia watu walipoongea naye. Pia karatasi hiyo iliniambia jinsi Mungu alivyoponya watu.

Ndipo nilijiuliza, “Ni fedha kiasi gani utawapa watu hawa utakapowaendea kwa ajili ya kuponywa?” Lakini niliona katika karatasi hiyo imeandikwa, “Mpe Bwana mizigo yako, naye ataibeba.” Baada ya kusoma hivyo, niliamua kusema na Mungu kwa ajili ya shida zangu. Niliamini kuwa angeweza kuponya miili ya watu. Hali kadhalika, niliona kwamba aliwaruhusu watu wamwue Mwanawe Yesu Kristo kama adhabu ya dhambi za watu. Nilimwomba anisamehe dhambi zangu.

Nilipoamka asubuhi iliyofuata nilitazama mwili wangu nao uvimbe ulikuwa umetoweka. Sura yangu ilirudi kama ilivyokuwa mwanzoni. Ndipo nilipopiga kelele, “Nimepona, Mungu ameniponya!!!” Sasa nawaeleza kila mtu kwamba mambo yanayoandikwa katika UPESI ni kweli kabisa nami nimethibitisha kuwa Mungu anaponya hata sasa.

Nime kwisha kataa maovu

na Ibo Ismelene — Guadeloupe

Mimi ni mwanamke wa Guadeloupe na kwa miaka minne nilitembea na mvulana Mfaransa ambaye alihudumia nchi yetu kama mwana Jeshi. Ndani yangu kulikuwa na nguvu ambayo ilinikataza kufanya uasherati kwa kuwa nilikuwa mkatoliki. Tulifanya hata mambo yote ya karamu ya kawaida kwa msichana kuyatenda kabla ya kuolewa.

Wakati huo mamangu alinishauri nifuatane naye katika kanisa la Kiinjilisti. Nilikataa kwani sikupenda kushiriki katika dini nyingine. Mamangu aliponiombea Bwana Yesu alinibadilisha kimwujiza. Badiliko hilo nilipata mwaka uliopita. Sasa nimeokolewa kabisa nami ninalo tumaini katika Bwana, nami namshukuru sana.

Mvulana huyo nilivyokuwa nimetembea naye hakuelewa kwa nini nimegeuka kuwa mtoto wa Mungu. Sitembei tena naye kwa sababu nimekwisha kataa maovu yote. Sasa wengine wanatambua kuwa Mungu anaishi ndani yangu nami namfuata Yesu sasa.

Kata hapa

Jina .....No 78/.....

Anwani .....

.....

Nchi.....

KWA KUPEWA NAKALA YA UPESI BILA MALIPO, Andika jina na anwani yako hapa kwa HERUFI KUBWA.
Mtumie: Mr. David M. Eunson, Administrator, Bowstones, Hall Crescent, Gullane, East Lothian, EH31 2HA, Scotland, UK

Nilikombolewa toka nguvu za uchawi

na I.M.
Switzerland

Mama yangu alikuwa mshirikina naye alinipeleka kwa wachawi na walozi. Mara kwa mara nilishikwa na majinamizi na pia nilikuwa na mawazo ya kujiua. Uhusiano wangu na mama kama mwanamke na binti yake ulikuwa mbaya sana. Nilipokuwa mtoto mdogo sana nilianza wizi ingawa familia yetu ilikuwa ni ya kitajiri, kisha nikageuka kuwa jambazi. Nikaanza kuteseka kwani sikupata usingizi zaidi ya masaa mawili ya usiku. Hali hiyo iliendelea kwa miaka mingi hadi nilipofikisha umri wa miaka thelathini.

Wakati huo jirani mmoja alianza kuomba sana kwa ajili yangu. Alinizingira kwa upendo mwingi na uvumilivu. Akaendelea kwa bidii kunieleza habari za Yesu Kristo na pia jinsi anavyonipenda naye angeweza kweli kweli kunisaidia. Baada ya siku chache nililala usingizi usiku kucha nami nilipoamka nikiwa nilijisikia vizuri. Ilikuwa mara ya kwanza kabisa katika maisha yangu kujua furaha na amani ya kweli.

NILIVICHOMA VITABU VYANGU

Huyo rafiki alinieleza kuwa ningeweza kuongea na Yesu kama rafiki kuhusu mambo yote ya maisha yangu. Basi nilitubu na kuomba msamaha wa dhambi zangu zote kwa Mungu na wale walionizunguka. Furaha na amani iliongezeka, hasa kwa sababu nilikuwa na mzigo moyoni mwangu, kwa kuwa kabla ya kumpokea Yesu nilitoa mimba. Nilichoma vitabu vyangu vyote vya uchawi kwani sikuvihitaji tena. Nikavirudisha vitu nilivyoiba toka dukani. Kwa muda wa miaka mingi mimi na babangu tulikuwa hatuongei na kwa wakati huo baba aliugua na kansa. Baada ya kupatana naye nilimwombea, naye alipona kabisa. Kwa kweli kuna nguvu katika msamaha na maombi yanayofanywa kwa jina la Yesu Kristo.

Kwa miaka ishirini sasa nimekuwa nikihudhuria kanisa lakini mwanzoni niliona ni vigumu sana kusoma Biblia na kuomba kila wakati. Nilikuwa na visingizio vingi: watoto watatu, nyumba, bustani na kadhalika. Na hata wakati ambapo nilipata muda, sikuomba wala kusoma Neno nikidhani kuwa ningeweza kuendelea na maisha ya kikristo kwa nguvu zangu. Hivyo ilikuwa kujidanganya kabisa. Nilianza tena kuanguka katika dhambi zangu za awali. Maisha yangu ya kiroho yakawa matupu sana na nikakosa furaha.

Kisha usiku mmoja nilinyenyekea mbele ya Mungu na kutua mzigo wa moyo wangu. Nilitambua kuwa ningeweza kukua vizuri kama nikisoma Neno la Mungu na kuomba kila siku. Bwana asifiwe kwani alisema, **“Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.”** (Yohana 15:5)

Sasa nina furaha ya kweli

na Sivamwenda Lewis Molo
Jamh. Kidem. ya Congo

Mama na babangu hawakuamini lolote. Mimi niliamua kuishi kama wazazi wangu nami sikupendelea mambo yoyote ya dini. Tangu nilipokuwamo Shuleni mwa Msingi niliamua kufanya mambo mengi ya dunia. Yalikuwa ni mambo ya kiuhuni ambayo yalinifanya nikose amani. Nilipotea kabisa katika njia nyingi za upotevu.

Lakini namshukuru Mungu aliyenitafuta. Katika umri wangu wa miaka 17 niliacha vyote nami nilimfuata Yesu Kristo ambaye alijitoa kwa ajili yangu, nazo dhambi zangu alizisulubishwa msalabani. Tangu nilipompokea Kristo nimekwisha kupata furaha ya kweli kwani Yesu alinibadilisha. **“Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya;”** (2 Wakorinto 5:17a) **“Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu;”** (Wagalatia 2:20a). Mungu anao mpango maalum kwa ajili ya maisha yangu kwa kuwa alisema, **“Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema BWANA, ni mawazo ya amani wala si ya mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho.”** (Yeremia 29:11)

Nilipaswa kutafuta jibu

na Mulama Mozart
Jamh. Kidem. ya Congo

Hadi niliposoma ushuhuda mmoja katika gazeti la UPESI sikuelewa maana ya wokovu. Nilikosa uwezo wa kumtumikia Kristo wala sikuwa na kiu ya kumshuhudia Kristo kwa wengine. Sikusimama imara katika Neno la Mungu na kuhubiri Injili kwa sababu mimi sikuwa mwamini. Niliokoka kuwa Mkristo mwaka wa 1984 na tangu nilipoamua kumpokea Kristo maishani mwangu, nimesimama imara.

Nilipokuwa kijana nilikuwa mwimbaji mzuri sana kanisani. Kila nilipoimba watu walishangilia. Kuimba kanisani pamoja na kuzaliwa katika jamaa ya Kikristo kulikuwa maana ya wokovu kwangu. Hata hivyo, maisha yangu yalikuwa mabaya sana, na hata nilishindwa kupita mitihani yangu ya kitaifa.

MAMBO YALINIPINDUKIA

Wakati huo kasisi wangu alinipa ‘maji matakatifu’ lakini hayakunitakasa. Nilikuwa nimemwasi Mungu na Neno lake. Niliwapenda wanawake, nilikunywa pombe ili niweze kulala usingizi na kwa sababu hii mambo yote yalinipindua kila wakati.

Siku moja nilijua kuwa ilinibidi nilitafute jibu la matatizo haya, lakini, je, ningefanyaje? Ndipo ndugu yangu akanipa karatasi ya UPESI nami nikaokoka. Ninao ndugu na rafiki wengi ambao bado wanatembea katika giza nao wana haja ya kuja kwenye Nuru. Kwa hiyo sasa nafanya kazi ya kuwaleta kwa Yesu.

Yesu alituahidi:

“Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo.” (Yohana 14:1-3)

REDIO HABARI MAALUM

S.L.P. 7292, ARUSHA TANZANIA

Ukitaka Masomo ya Biblia kwa njia ya posta agiza kwa anwani hio.

KILA SIKU

SAA	J’PILI	J’TATU	J’NNE	J’TANO	ALHAMISI	IJUMAA	J’MOSI
ASUBUHI 12.15–12.45	NENO LA UZIMA (spots)	BIBLIA INAJIBU	HABARI NA MASOMO	NYIMBO NA SALAMU	PICHA ZA MAISHA (RHM-Club)	TUME-ONANA	MAFANIKIO BORA
USIKU 1.15–1.45	TUME-ONANA	NYIMBO NA SALAMU	SIKILIZA TUKUAMBIE (Mashindano)	MSAADA NJIANI	BIBLIA INAJIBU	REHEMA NA NEEMA	TUWE PAMOJA

Ukitaka kupata Masomo ya Biblia katika lugha ya Kiswahili kwa posta, tuma jina lako na anwani yako kwa:

Katika KENYA: Evangel Bible Courses, SLP 28963, Nairobi, Kenya.

Katika CONGO: Cours Biblique Emmaus, BP 350 Bunia, Rég. du Haut-Congo, Jam. Dem. ya Congo.

Katika TANZANIA: Emmaus Shule ya Biblia, SLP 9322, Dar-es-Salaam, Tanzania, inasubiri barua yako ili uweze kutumiwa somo la kwanza bila malipo.

Kwenye MITA BENDI 25

Vipindi vitasikika kwenye MITABENDI 31